


**Kituo cha usajili na kupanga wanafunzi
kiko wapi?**

999 N. University Drive
(North of Downtown)
Fort Worth, TX 76114
Phone: 817.815.7700
Email: spc@fwisd.org



Fort Worth ISD inakataza ubaguzi, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji, dhidi ya mfanyakazi yeyote kwa msingi wa Ukoo, rangi, dini, jinsia, asili ya taifa, umri, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu, utambulisho wa kijinsia na kujieleza, hali ya kijeshi/mkongwe, au msingi mwingine wowote unaokatazwa na sheria. Kulipiza kisasi dhidi ya mtu yeyote anayehusika katika mchakato wa malalamiko ni ukiukaji wa sera ya Wilaya. Mtu huyu ameteuliwa kushughulikia maswali kuhusu sera za kutobagua: Cynthia Allen, Mratibu wa Kichwa cha IX, 7060 Camp Bowie Blvd., Fort Worth, TX 76116, 817.814.1837, Barua pepe: TitleIX@fwisd.org



Swahili

¡Bienvenidos!

Soo dhawow!

**Svāgata
cha!**

**'ahlaan
bk!**

Kyaosopaartaal!

Karibu!

Student Placement Center

Fort Worth Independent School District

Kituo cha kuwapanga wanafunzi ni nini haswa?

Kituo cha kuwapanga Wanafunzi katika mashule cha Fort Worth ISD hutoa msaada kwa familia mpya ambazo hazijawahi kusajiliwa katika shule ya umma ya Texas na ambao huzungumza au kusikia lugha nyingine isipokuwa Kizungu. Kituo hicho hupeana huduma za usajili na huwasaidia wanafunzi ili wawe na mwaka shuleni wenye mafanikio kimasomo.

Je, wanafunzi wote wapya wanaongea lugha Zaidi ya Kiingereza wanahitaji kufanyiwa mtihani?

Ikiwa swali lolote kati ya matatu yaliyo hapa chini yamejibiwa kwa lugha nyingine isipokuwa Kizungu NA mwanafunzi hajawahi kusajiliwa katika shule ya umma ya Texas basi jibu ni "Ndiyo".

- Ni Lugha zipi zinazotumika nyumbani?
- Ni lugha gani zinazotumiwa na mtoto nyumbani?
- Kama mtoto alikuwa na mpangilio wa nyumbani hapo awali, ni lugha gani zilizotumika? Kama hapakuwa na mpangilio wa nyumbani hapo awali, jibu Not Applicable (N/A).

Kujiandikisha/Usajili utachukua muda gani?

Muda utatofautiana kutoka dakika 45 hadi saa 2.5, kulingana na gredi la wanafunzi na alama alizopata. Wanafunzi wa umri wa shule ya msingi wanaweza kupangwa asubuhi sana au alasiri, kwani mitihani hizi si ndefu kama za wanafunzi wa umri wa sekondari.

Ni rekodi gani zinazowahusu wanafunzi ambazo wazazi wanapaswa kuleta katika Kituo cha kuwapanga Wanafunzi?

- Uthibitisho wa umri na utambulisho wa mwanafunzi
- Rekodi ya sasa ya chanjo
- Kitambulisho ya Mzazi/Mlezi
- Uthibitisho wa unakoishi
- Kadi ya ripoti au Hati ya Kimataifa (aina yoyote ya rekodi za shule kutoka shule ya awali, zinazotumika)
- Uthibitisho wa hali ya Asyle/Mkimbizi (hati ya mrithi, ikiwa inapatikana)

Wazazi wanaweza kutuma hati zinazohitajika kwa barua pepe kutumia kompyuta:
SPC@fwisd.org

Jeh, wazazi wanahitaji kupanga mkutano?

Ndiyo, mkutano itapangiwa kwa kupiga simu Kituo cha Upangaji wa Wanafunzi kwa 817.815.7700 au mshiriki wa timu ya SPC atawasiliana na mzazi.

Masaa ya kazi ni yapi?

Kituo kinafunguliwa kuanzia saa 8:00 asubuhi . thadi 5:00 jioni. Jumatatu-Ijumaa, bila kuhesabu siku za likizo.

Wazazi wanafaa kutarajia nini wakienda kwenye kituo cha kujiandikisha/usajili na kupanga wanafunzi?

Wazazi wanaweza kutarajia:

- kukaribishwa na wafanyakazi wanaozungumza Kizungu, Kihispania na lugha zingine (wakalimani wanapatikana wanapooombwa waje)
- kupokea taarifa/msaada kwa:
 - Usajili wa wanafunzi
 - Mtihani ya kupangwa kwa wanafunzi
 - Habari za programu ya lugha mbili/Kizzungu
 - Tafsiri za kimataifa za nakala
 - Habari za basi
 - Habari za chanjo
 - Habari za ISD za Fort Worth (sheria za mavazi, lango kuu, n.k.)
 - Mwelekeo wa mzazi/mwanafunzi
 - Huduma za mthibitishaji
- Utaondoka kwenye kituo cha usajili na bahasha ya njano inayohusu taarifa za uandikishaji kwa shule uliyopewa (hati zozote za uandikishaji zinazopatikana zinapakiwa kwenye kompyuta ya usajili mtandaoni)
- huduma za ufuatiliaji kuhusu tafsiri ya nakala za kimataifa, usaidizi kuhusu masuala ya usafiri, au maswali mengine yanayohusiana na shule

Kuna malipo yoyote kwa huduma utakazopokea kwenye kituo?

Hapana, Fort Worth ISD inapeana huduma hizi bila malipo yoyote.